DA YA

SKAZINI



# Magugu vamizi yaathiri mifugo, wanyamapori

Mussa Juma,Mwananchi
mjuma@mwananchi.co.tz

**Arusha.** Wafugaji wilayani Longido na wilaya za jirani mkoa wa Arusha na wahifadhi, wameanza kukabiliwa na upungufu wa maeneo ya malisho kutokana eneo kubwa la ardhi kuvamiwa na magugu vamizi ambayo hayaliwi na wanyama.

Uchunguzi uliofanywa na *Mwananchi* umebaini zaidi ya ekari 20,000 za malisho ya mifugo na wanyamapori zimevamiwa katika maeneo ya wafugaji na hifadhi za wanyamapori katika mkoa wa Arusha.

Kutokana na uvamizi huo, tayari jitihada zimeanza kuchukuliwa kukabiliana na uvamizi huo, ambao unatishia maisha ya wanyama na kuanza kuathiri uchumi na kuongeza umasikini.

Akizungumza na *Mwananchi*, Mkurugenzi wa shirika la Utafiti na huduma za jamii (CORDS), Lilian Looloitai alisema magugu vamizi ni sehemu ya athari za mabadiliko ya tabia nchini,hadi sasa yameathiri nyanda za malisho kwa kiasi kikubwa.

Alisema ili kukabiliana na changamoto hiyo, shirika kwa kushirikiana na Serikali, wamezindua mradi wa uboreshaji nyanda za malisho ambao utaanza katika vijiji saba wilaya ya Longido.

Alivitaja vijiji hivyo ni Mundarara, Orgira, Olpukai, Olbomba, Oltepesi, Oldonyo na Leremeta ambapo wananchi watapewa elimu ya kukabiliana na magugu vamizi lakini pia kuzuia athari zaidi za mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Ha almashauri ya Longido, Jumaa Mhina aliagiza viongozi wa kata na vijiji kushirikiana na wananchi kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi katika wilaya hiyo.

Magugu hayo pia yamevamia maeneo ya hifadhi ikiwepo eneo la Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro.

MSAADA

Scanned with CamScanner

# Wakulima, wafugaji wauana Lindi

**Na Said Hauni, Lindi**

**TABIA** ya baadhi ya viongozi wa Serikali wilayani Kilwa, mkoani hapa kupuuza taarifa na malalamiko ya wananchi, imeanza kuleta majibu hasi, baada ya kuibuka mapigano yaliyosababisha vifo vya watu watatu katika kijiji cha Nanjilinji 'B'.

Vurugu hizo zilisababisha vifo vya wafugaji wawili na mkulima, Julai 20 mwaka huu, kati ya saa tano na sita adhuhuri, baada ya kundi la wafugaji kudaiwa kugeuza shamba la Chande Magoma, kuwa malisho ya mifugo. Mapigano hayo yanayoelezwa kuchukua takribani siku mbili, yalizimwa na polisi waliofika kijijini hapo kutuliza vurugu hizo.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, wakizungumza kwa masharti ya kutotajwa majina, walidai kuwa sehemu kubwa ya vurugu hizo, ilichangiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, kupuuza malalamiko ya wananchi juu ya matatizo wanayopata kwa wafugaji.

Wakifafanua, wakazi hao walidai kwamba matokeo ya vurugu na vifo hivyo ni majibu kwa Ofisi hiyo kutokana na kutotekeleza ipasavyo malalamiko waliyopeleka kwa watendaji hao wa Serikali ngazi ya wilaya.

Aidha, walieleza kwamba kuanzia mwaka juzi kupitia kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Kassimu Maimula, walikuwa wakipeleka taarifa na malalamiko kwa uongozi wa wilaya, kuomba uondoe wafugaji baaqda ya kuchoshwa na hasara kutoka kwa wafugaji kugeuza mazao yao malisho ya ng'ombe wao.

Walidai kwamba licha ya kupeleka taarifa hiyo takribani mara tatu, hakuna jitihada zilizofanyika, hadi vurugu zilipoanza na kusababisha vifo vya watu watatu, wakiwamo wafugaji wawili na mkulima mmoja.

"Kipindi tulichopeleka malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya alikuwa aliyeachwa katika uteuzi mpya wa Rais Samia Suluhu Hassan," alieleza mmoja wao.

Julai 20 mwaka huu, watu watatu akiwaqmo mkulima Magoma na wafugaji wawili, ambao majina yao bado hayajafahamika, walipoteza maisha katika mapigano Nanjirinji 'B'.

Mapigano hayo yanadaiwa kuchangiwa na kundi la wafugaji kupeleka mifugo kwenye shamba la Magoma kula mahindi yaliyokuwa hayajaondolewa, hali iliyozusha vurugu zilizosababisha mauaji hayo.

Kwa mujibu wa taarifa za wakazi wa Nanjirinji 'B', Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa alifika kijijini hapo na kuwataka wananchi waendelee kutulia, wakati uongozi ukiendelea kutafuta utatuzi wa changamoto zao.

Hata hivyo, mwandishi alipomtafuta Mkuu kupitia simu yake ya mkononi, ili kupata kauli yake juu ya vurugu hizo, iliita bila kupokewa.

Raia Mwema Uk.6, Tarehe 27/07/2021

Scanned with CamScanner

wa Ufupi



**Ubaguzi bado tatizo kwa wenye VVU**

**Dodoma.** Ubaguzi na unyanyapaa ni miongoni mwa sababu zinazochangia vijana wengi wanaoishi na virusi vya Ukimwi kutokwenda vituo vya kutolea huduma za afya.

Akizungumza jana Mtaalamu wa masuala ya jinsia na maendeleo ya jamii, Dk Katanta Simwanza alisema tafiti zinaonyesha kundi hilo la vijana wenye umri katia ya miaka 15 hadi 25 halitaki kwenda vituo vya kutolea huduma na miongoni mwa sababu ni kuogopa unyanyapaa. Mratibu wa Programu za Ukimwi na Jinsia kutoka UN Women, Jacob Kayombo alisema ili kukabiliana na changamoto hizo kwa kushirikiana

MAPIGANO

# Mgogoro wa wafugaji waua mmoja, wanne wajeruhiwa

**Lilian Lucas**, Mwananchi
llucas@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Vurugu zilizoibuka katika kijiji cha Tindiga wilayani Kilosa baina ya wafugaji wa jamii ya kimasai na wa kisukuma, zimesababisha kifo cha mtu mmoja, John Nyerere na wengine wanne kujeruhiwa.

Mauaji hayo yanadaiwa kutokea baada ya wafugaji wa jamii ya kisukuma kuwatuhumu wenzao wa kimasai kutaka kuiba mifugo yao.

Kutokana na mauaji hayo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela akiongozana kamati yake ya ulinzi na usalama ya mkoa walifika na kuwasihi wananchi kuwa watulivu wakati vyombo vya dola vikifuatilia na kuchukua hatua kwa watuhumiwa wote waliohusika na mauaji hayo.

Shigela aliliagiza jeshi la Polisi kuwatafuta wahusika na alieleza kuwa wanafahamika na kama ndugu wasipotoa ushirikiano wakamatwe wao.

"Kila siku nitauliza waliokamatwa, Serikali lazima tukomeshe hii tabia. Nawapa pole wale wote waliofikwa na msiba na majeruhi," alisema Shigela.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim alisema kwa taarifa zilizoripotiwa Polisi chanzo cha vurugu hizo ni kundi la wamasai kwenda kuiba ng'ombe na kwamba wakati wanawaswaga ndipo yalipozuka mapigano.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 24, saa 12 jioni katika kijiji cha Tindiga baada ya mvutano wa wafugaji wa kimasai kutaka kuchukua kwa nguvu mifugo iliyokuwa machungoni ya mfugaji wa kisukuma.

Muslim alisema watu 19 wanatafutwa kwa tuhuma za kuhusika na vurugu na mauaji na wakikamatwa watafikishwa mahakamani.

**04** Jumla ya watu walijeruhiwa katika mapigano hayo.

**19** Idadi ya watu wanaosakwa na polisi wakituhumiwa kuhusika katika vurugu.

Mkazi wa kijiji cha Tindiga, Said Kindamba alisema wafugaji wametawala katika maeneo hayo na kwamba kesi zimekuwa zikiripotiwa, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

"Tunachoomba viongozi wetu wa juu wachukulieni hatua wanaosababisha haya yote hasa viongozi wa vijiji," alisema Kindamba.

Naye mkazi wa Tindiga, Mohamed Msilimu alisema kumekuwa na vurugu za muda mrefu katika eneo hilo, lakini kutokana na kufumbiwa macho na baadhi ya viongozi waliopita ndo kumesababisha mapigano makubwa kutokea.

Alisema vurugu si kwa wafugaji pekee, bali hata wakulima na wafugaji zimekuwa zikitokea kutokana na mashamba yao kulishwa mifugo hasa kipindi cha kilimo.

Katika hatua nyingine, Shigela aliagiza kukamatwa kwa Nassoro Nzige anayetajwa kuwa kinara wa kupanga njama na wafugaji, ili kulisha mifugo kwenye mazao ya wakulima.

Shigela alisema mwananchi huyo na wenzake wamekuwa wakipita shambani na baadaye kwenda kwa wafugaji kupewa fedha na nyingine kuwapatia askari, hivyo wafugaji wanapokamatwa wanarudishwa na kuanza kujitapa kwa wananchi.

Scanned with CamScanner